

# CHOCHEA KIPAJI CHAKO

Daudi Lubeleje

Kitabu hiki ni maalumu kwa wote wenye kiu ya kutumia vipaji vyao. Ni maalumu kwa wote wanaotaka kutumia vipaji vyao bila kuharibu uhusiano wao na Mungu. Kitabu chote kimejaa kanuni na mbinu muhimu za kukusaidia.

# YALIYOMO


**UTANGULIZI** ........................................................ 6
**SURA YA KWANZA** .................................................. 9
Kipaji
Mambo 4 kuhusu kipaji
Kuna ngapi za vipaji?
Tofauti ya Karama na Kipaji

**SURA YA PILI** ........................................................ 18
Njia 4 za kugundua kipaji chako

**SURA YA TATU**........................................................ 23
Mbinu za kuchochea kipaji chako
Sababu 2 uchochee kipaji chako

**SURA YA NNE** ........................................................ 27
Badili chanzo chako cha taarifa
Funzo kutoka kwa shujaa Gideoni
Jifumue, Anza upya

**SURA YA TANO** ..................................................... 33
Badili watu unaombatana nao
Watu waliokosea kuchagua watu wa kuambatana nao
Unachaguaje mentor wako?

**SURA YA SITA** ...................................................... 40
Ongeza maarifa/Ujuzi
Tabia moja muhimu

**SURA YA SABA** ..................................................... 45
Jiandae nyuma ya pazia

**SURA YA NANE** .................................................... 49
Maombi

**KUHUSU MWANDISHI** ........................................ 53
**KUHUSU KITABU** ................................................ 55

# SHUKRANI

Kutumia kipaji changu cha uandishi na kuwafikia wengi kupitia maandishi ni matokeo ya kazi njema ya Mungu kunivumbua na kunitengeneza; Hakika sifa, utukufu na shukrani nyingi anastahili Mungu.

Nawashukuru wazazi wangu Mr & Mrs Jonasi Lubeleje kwa sapoti yao kwangu isiyokoma. Pia namshukuru Mchungaji wangu, Godfrey Mwaifani na washirika wote wa kanisa la EAGT- SANAWARI, Arusha kutambua kipaji nilichonacho na kunipa nafasi ya kufundisha kuhusu kipaji kwa mara ya kwanza, na ndipo wazo la kuandika kitabu hiki likazaliwa.

Kipekee kabisa, natambua mchango wa rafiki yangu Elibaraka Mmari na kwa sapoti yake kubwa. Bila kusahau, nakushukuru sana wewe mdau wangu kwa kukubali kununua kazi yangu na kuwa mfuatiliaji wa kazi zangu za uandishi.

Mwisho kabisa, nawashukuru wote waliofanikisha kazi hii kukufikia, ni wengi kuwataja na ninatambua mchango wao.

# UTANGULIZI

Maisha yamebadilika sana katika ulimwengu wa leo. Watu wengi sana wenye vipaji wanatengeneza hela nyingi kupitia vipaji vyao tofauti na miaka ya nyuma. Tukirejea miaka ya nyuma watu wenye vipaji walikuwa wanaonyesha vipaji vyao bure kabisa na ushindani ulikuwa haupo. Ni kama kusema mtu wenye kipaji alikuwa haingizi hela yoyote, na ikitokea ni kiduchu tu ya kupewa pongezi.

Hali imebadilika miaka ya hivi karibuni, watu kama MC Pilipili, Samweli Sasali, Dr. Chris Mauki tayari wamewekeza kwenye vipaji vyao vya ushehereshaji na wanalipwa pesa nyingi kwa masaa machache tu. Kwa upande wa uandishi wa vitabu, kuna wimbi la waandishi vijana walioibuka kwa kasi kama uyoga na wanaandika vitabu na kupata pesa nyingi. Wako waandishi vijana wa vitabu ambao hata mimi najifunza kwao, kuwataja wachache tu; kuna Emmanuel Makwaya, Kelvin Kitaso, Shemeji Melayeki na Fred Msungu. Wapo waimbajiwa muziki wa injili kama Paul Clement, Jesca Honore, Angel Sakafu, Sarah Ndossi wanaofanya vizuri sana kwa ubora. Badiliko hili linaonyesha namna hali ilivyobadilika kwa sasa, kipaji imekuwa ni pesa. Haya yote yamevutia wengi kuanza kutumia vipaji vyao na ushindani kuongezeka. Ukitumia kipaji chako, si tu utafanya kwa ubora bali pia ni muhimu kuonyesha upekee na utofauti wako. Kuna wengine wamezamia kwenye vipaji visivyo vyao, na wanaotaka kufanikiwa kupitia vipaji vya wengine kwa kuishi maisha ya kuiga wameongezeka pia.

Kitabu hiki kimelenga kukupa maarifa ya kukusaidia kufanya vizuri kwenye kipaji chako katika ulimwengu huu wa ushindani. Kina kanuni za kumsaidia mwenye kipaji kufanya vizuri zaidi. Tunaishi sasa kwenye ulimwengu wa taarifa; kwa kadiri unavyopitwa na taarifa sahihi ambazo ulitakiwa uwe nazo, ndivyo unavyokuwa mbali zaidi na kufanikiwa. Mtu anayetengeza pesa kupitia kipaji chake hapitwi na taarifa muhimu, kila mara anaongeza maarifa mapya. Kujiongeza thamani ni suala lisilokwepa kwa mwenye kipaji na kati ya jambo muhimu kushughulika nalo ni kuongeza maarifa. Nimeelezea mambo kadhaa yatakayoongeza thamani yako na kukufanya uanze kufanya vizuri kwenye kipaji chako.

Kuna watu wanaishi bila kujua vipaji vyao. Wanakosa pesa ambazo kama wangejua vipaji vyao na kuvitumia, maisha yao yangebadilika kabisa. Kuna nyimbo tunazikosa kwa sababu kuna mtu hajui ana kipaji cha kuimba, kuna vitabu tunavikosa kwa sababu kuna mtu hajui ana kipaji cha uandishi. Sura ya 2 ya kitabu hiki zimeelezwa mbinu 4 za kukusaidia kugundua kipaji chako. Utakapomaliza kusoma kitabu hiki, utaanza kutumia kipaji chako, kwani kiuhalisia; aliwahi kusema Mchungaji Raphael *"Umeumbwa uwe mkuu kwa kuwatumikia watu kupitia kipaji chako".*

Kutumia kipaji chako ni huduma kwenye mwili wa Kristo. Kila unapotumia kipaji chako ni utumishi. Kanisa linahitaji watu wanaotumia vipaji vyao. Kila mwamini akisimama katika zamu yake, basi kupitia vipaji vyetu tutahudumiana. Ieleweke kwamba, Pesa zitakuja tu unapotumia kipaji chako, kwa hiyo lengo lisiwe tu kutengeza pesa kwani kuna vijana wengi ambao kutumia vipaji vyao

kumewatoa kwenye uwepo na Mungu. Kwa bahati mbaya hata baada ya mtu kuharibu mahusiano yake na Mungu kipaji chake huendelea kufanya vizuri. Hujawaji kuona watu wakiwa na ushirika mzuri na shetani na vipaji vyao vinaendelea kuwapa pesa nyingi?. Yote yaliyoelezwa ndani ya kitabu hiki, yanalenga kumfanya kijana atumie kipaji chake na mahusiano yake na Mungu yazidi kukua.

Lengo mahsusi la kitabu hiki ni kukufanya wewe uanze kuchochea kipaji chako kwa kujifunza mbinu zilizoelezwa humu na kwa kufanya hivyo utaanza kufanikiwa na kupanda kwenda juu katika maisha yako ya kipaji.
Daudi Lubeleje,
Mwandishi wa kitabu,
Arusha, Tanzania.



# SURA YA KWANZA

# KIPAJI

> Kipaji ni zawadi ambayo huja na wajibu wa kuwatumikia wengine na sio kwa ajili yetu sisi wenyewe kwa sababu hatujajipa wenyewe

— Jose marti

Kwa kawaida neno la kiingereza "Talent" ndilo hutafsiriwa "kipaji"kwa lugha ya Kiswahili. Neno jingine ni "*gifts*" ambalo, pia hutafsiriwa kipaji. Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili TUKI toleo la pili la mwaka 2000, inatoa tafsiri ya neno "gifts" kuwa ni"*zawadi, hiba, tunu*". Kipaji ni zawadi. Kipaji mtu huzaliwa nacho, kwa hiyo tunaweza kusema *"kipaji ni zawadi mtu anayozaliwa nayo".* Mtoaji wa kipaji ni Mungu na hutoa kwa kila mtu. Unazaliwa kipaji ukiwa nacho, kazi yako kubwa ni kugundua kipaji chako ni kipi. Katika sura ya 2 tutaona njia 4 za kugundua kipaji chako. Ni ukweli kuwa wengi wetu hatujui vipaji tulivyonavyo. Kwa bahati mbaya hatufanyi juhudi kujua. Kupitia njia hizi 4, utaweza kujua kipaji chako, na huo ni mwanzo mzuri kuanza kukitumia kwani huwezi kitumia kitu usichojua.

Kipaji ni uwezo wa kipekee/maalumu Mungu awekao ndani ya mtu ili afanye jambo au mambo kwa ufanisi wa hali ya juu. Ufanisi huu, huwa hauwezi kufikiwa kwa hali ya kawaida.

Kipaji ni kama upendeleo wa kipekee, mtu apokeao Kwa Mungu bila kulipa gharama fulani. Bwana Yesu aliwahi kusema;"*Mmepata bure*………………".Upendeleo huu wa Ki - Mungu humpa mtu kukubalika katika mioyo ya watu bila mtu mwenyewe kutumia nguvu yoyote. Kwa wanaotambua kuwa vipaji vimewatengezea nafasi, basi huzitumia nafasi hizi kwa faida.

Kipaji ni uwezo uliowekezwa ndani ya mtu na Mungu mwenyewe ili huyo mtu atumike vizuri kwenye eneo/uwanja fulani Mungu aliompa. Eneo la kipaji chako ni kama uwanja wa nyumbani, mafanikio yanakuja tu bila hata kuhangaika sana. Nimnukuu Samweli Sasali, aliwahi kusema "*unafanya jambo pasipo nguvu kubwa, kwa ufupi kipaji ni kama quick software ambayo inakufanya uwe wa kipekee sana"*.

Kati ya watu ninaowafwatilia kwa ukaribu kwenye mtandao wa facebook ni Mwalimu na Mchungaji Dickson Kabigumila, Kiongozi wa makanisa ya Assembly of Believers Church (ABC). Mchungaji Dickson kwenye moja ya post zake aliwahi kuandika maneno haya;*"Anga ni kubwa sana kwa kila Nyota kuonekana na wala Nyota moja haijawahi kuizuia nyingine kung'aa".* Mtu mwingine kuwa na kipaji kama chako haikuzuii wewe kufanya kama wewe kwenye eneo lako. Hata vipaji vikifanana bado namna ya kuvitumia itatofautiana, na hii ndio maana ya kusema;"kila kipaji kina uwanja wake, na kinampa nafasi mwenye nacho kujidai kwenye uwanja wake"

Maswali ya kujiuliza; Kipaji changu ni kipi? Nakitumia kipaji changu? Kukijua na kukitumia ni mambo mawili tofauti; Kijue na kukitumia kipaji chako, hujachelewa!

## MAMBO 4 KUHUSU KIPAJI

Kama nilivyosema awali kuwa kipaji mtu huzaliwa nacho; na mtoaji wa kipaji ni Mungu, kwahiyo Mungu akikupa kipaji kwa tafsiri nyepesi kakupa uwezo wa kipekee kwenye eneo fulani ufanye vizuri na kwa ubora.
Yapo mambo 5 kuhusu kipaji nataka tuangalie hapa, ili yatupe uwanja mpana wa kuelewa kuhusu kipaji kwa kadiri tunaendelea kwenda kurasa za mbele.

## KIPAJI KIMEBEBA MAFANIKIO YAKO, KITUMIE

Nikimnukuu Mfalme Sulemani, mwandishi wa kitabu cha Mithali na Mhubiri, anasema; *"Kipawa ni kama kito cha thamani machoni pake yeye aliye nacho; Kila kigeukapo hufanikiwa" (Mithali 17:8),* Kwahiyo Mungu amekupa kipaji ukitumie, na unapoanza kukitumia tu (kila kigeukapo) unaanza kufanikiwa. Usipofanya mchakato wa "kila kigeukapo (yaani kukitumia)" yale mafanikio yaliyoambatanishwa na kipaji chako huwezi kuyaona. Rafiki yangu Bedon Dickson, Mkurugenzi wa Taasisi ya Growth Institute aliwahi kusema;*"Unaweza kuwa na hela nyingi kupitia kipaji chako. Ukiwekeza kwenye kipaji chako unaweza kutengeneza pesa nyingi sana"*. Kuwekeza kwenye kipaji ni;"kukifanya kila kigeukapo kikupe hela". Ni mchakato wa kujiongeza thamani kwenye kipaji chako.

## HAKIPATIKANI KWA KUNUNUA, UNAPEWA BURE NA MUNGU

Kipaji huwa hakinunuliwi, mtu huzaliwa nacho, ni zawadi ya Mungu kwa mtu. Kukinoa kipaji chako ni gharama ambayo kila mwenye kipaji hakwepi kuilipa. Tofauti iko kwa asiyenacho, hawezi kununua kipaji. Kwa lugha nyepesi, gharama hailipwi kwa kununua kipaji ila kwa kukinoa kipaji chako. Kwa mtu ambae hana kipaji, Mfano uchekeshaji, hawezi lipa fedha mahali fulani akapewa uwezo wa kuchekesha ila kwa aliye na hicho kipaji akitaka kujinoa zaidi itamhitaji kwenda shule (gharama).

Petro akimjibu Simoni, anamwambia;"*.....Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu (kipaji) yapatikana kwa mali"* (Matendo ya Mitume 8:20). Kila mtu ana kipaji. Kama hujui kipawa chako, jambo mojawapo la kufanya, ni kumwomba Mungu akupe kujua kipaji chako na siyo kutamani kipaji fulani ukatenga fungu la pesa kununua, utafeli!.

## HUWEZI KUKIKATAA/KUOMBA KUBADILISHIWA KIPAJI ULICHOPEWA NA MUNGU.

Warumi 11:29; *"Kwa sababu karama za Mungu (ikiwemo kipaji) hazina majuto.........*" [mkazo ni wangu]. Hili neno "hazina majuto" kwenye biblia za tafsiri ya kiingereza, limetumika kama; *"never be withdrawn"* (NLT) au "*irrevocable*" (AMP). Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili TUKI toleo la pili la mwaka 2000, inatoa tafsiri ya neno *"irrevocable*" kuwa ni;*siotenguka au siobadilika*. Tunapata maana gani hapa?, Kwa hicho kipaji ulichonacho, huwezi kujuta kwanini umepewa

hicho na sio kile kama cha fulani. Kuna mazingira huwa yanatokea, unaona kipaji chako ni duni na si bora kama cha fulani na kupelekea kutamani ungekuwa na kingine. Kujuta kwako, hakumfanyi Mungu kukubadilishia akupe kingine. Kipaji hakibadilishwi ila kinanolewa na kuwa bora zaidi. Kazi yako ni kuangalia utaanzaje kukitumia kipaji chako ili kikuletee mafanikio.

## KUJISIFIA KIPAJI KWA UONGO NI KAMA MAWINGU NA UPEPO PASIPO MVUA.

Kama huna kipaji fulani acha kujisifia kwamba unacho. Usiseme unajua kuogolea ilhali hujui na ukavuka mto uliofurika, matokeo yake utafeli vibaya sana. Joel Nanauka kwenye kitabu chake cha TIMIZA MALENGO YAKO anasema;*"watu wengi wanafeli kwa sababu wanafanya mambo katika sehemu ambazo hawajaumbwa kuwepo"*, Hii ni sawa na kujisifia kipaji kwa uongo ukijua kabisa huna uwezo huo. Tumia kipaji chako ulichonacho uone mafanikio, acha kupoteza muda kwenye eneo ambalo uwezo huna. Moja ya sababu inayofanya wengi kujisifia kipaji hewa ni kuishi maisha ya kuigiza. Ni kutaka kuwa kama fulani. Huu ni ulimbukeni kwani mwisho wa siku ni kama mawingu na upepo pasipo mvua

## KUNA AINA NGAPI ZA VIPAJI?

Kuna aina nyingi za vipaji kama ilivyo Nyota kwenye anga. Kipaji ni upekee. Watu wawili wanaweza kuwa wote wanaimba ila ule pekee unaowatofautisha ndio maeneo ya vipaji vyao. Kipaji ni uwezo unaokurahisishia kufanya mambo bila kutumia nguvu nyingi. Kipaji huambatana na ubunifu. Mfano, kuna wachezaji wengi wa mpira ila

hawafanani. Mchezaji mwenye uwezo fulani wa ziada, tunasema ana kipaji cha kipekee. Kwahiyo, kila mtu kwenye eneo lake, ana uwezo maalumu na kama akiutumia anafanikiwa kwa haraka sana. Ukifanya jambo fulani lililo nje ya kipaji ulichonacho unatumia nguvu nyingi sana. Unaweza ishia njiani kwa kukosa msukumo (passion) ya kuendelea kufanya. Mwenye kipaji anafurahia anachofanya, hachoki na haishii njiani.

## TOFAUTI YA KIPAJI NA KARAMA

Kila mtu ana kipaji, haijalishi mwenye nacho anajua au hajui, anakitumia au hakitumii, anaona kina thamani au hakina. Jambo moja la muhimu ni kuwa;"*huwezi kataa/kuomba kubadilishiwa kipaji ulichopewa na Mungu*" huko ni kupoteza muda!. Mwenye kazi ya kukipa thamani kipaji ni wewe.

Ipo tofauti kubwa ya kipaji na karama. Yako maeneo makubwa mawili (2) yaletayo utofauti wa kipaji na karama.

## ENEO LA KWANZA LA UTOFAUTI.

Kipaji kipo kwa wote; (a) Wasiomjua Mungu (*hawajazaliwa mara ya pili na kumfanya Bwana Yesu kuwa mwokozi wao kibinafsi)* na (b) Wanaomjua Mungu (wameokoka tayari). Kuna watu ambao hata hawajui mlango wa kanisa umeelekea wapi, ila wana vipaji na wanavitumia vizuri sana. Bwana Yesu aliwahi kusema kwenye hotuba yake, maarufu kama"*Hotuba ya mlimani*" *kuwa;".......maana yeye*

*(Mungu) huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki”* (Mathayo 5:45). Kipaji kimetolewa na Mungu kwa wote, bila kujali uhusiano wa huyo mtu na Mungu.

Karama haipo kwa watu wote, ipo kwa watu maalumu tu; waliompokea Bwana Yesu katika maisha yao. Unapoingia kwenye familia ya Mungu, kama asemavyo Yohana;*“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake”* (Yohana 1:12) mgawo wa karama hauwezi kukupita; unaweza kupokea!. Yale ambayo hungeweza kufanya kwa kukosa kipaji, ukiwa na karama unaweza kufanya. Kuna UONGOZI kama kipaji pia kuna UONGOZI kama karama. Hii ya pili, unapewa tayari umetengeneza uhusiano wako na Mungu.

Kila mtu ana kipaji. Umezaliwa na unaishi, basi ujue una kipaji bila kujali uhusiano wako na Mungu ni mzuri au mbaya. Kuwa na mahusiano mabaya na Mungu haiathiri kipaji chako, utaendelea kukitumia na kufanikiwa. Hivyo basi, kuna watu wengi wanafanya dhambi kwa ubora huku wakitumia vipaji na unashangaa kuona wanafanikiwa, isikupe shida, uwe umeokoka au hujaokoka vile unatumia kipaji chako ndilo jambo la msingi. ILA Karama ipo kwa waliotengeneza uhusiano wao na Mungu tu! Kwasababu, anayehusika na utendaji wa karama ni Roho Mtakatifu, Neno la Mungu linasema; *“Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule…….. lakini kazi (KARAMA) hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye” (1 Wakorintho 12:4,11)*

Kila aliyeokoka, ana faida mbili, ya kwanza; ana kipaji ambacho kipo kwa watu wote, ya pili; ana karama. Kila mwamini aliyejitambua hapa, utendaji wake sio wa kawaida; anafanya kwa viwango vya juu na kufanikiwa sana. Nikukumbushe tu, Mungu anataka ufanikiwe. Nimnukuu mchungaji Raphael Lyela, anasema kuwa;*"Kipaji hakihitaji uwe mtakatifu ili kifanye kazi; kama unabisha jipime na watu unaowaona ni wenye dhambi kwenye eneo hilo hilo la kipaji chako"*.

Kukitumia kipaji chako huku una Mungu ni faida kubwa kuliko uwe na kipaji huna Mungu. Bwana Yesu aliwahi kusema;*"utafuteni kwanza ufalme wake (wa Mungu) na haki yake....."pia akaongeza akasema;"itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akapata hasara ya nafsi yake?" (Mathayo 6:33, Marko 8:36)*

## ENEO LA PILI LA UTOFAUTI.

Kipaji mtu huzaliwa nacho. Maadamu umezaliwa basi una kipaji fulani. Kama unakumbuka niliandika; *"Kila mtu ana kipaji, haijalishi mwenye nacho anajua au hajui, anakitumia au hakitumii, anaona kina thamani au hakina"*

Mchungaji Raphael kwenye kitabu chake cha FICHUKA anaelezea NGUVU YA KUZALIWA kuwa ni; *"uwezo azaliwao nao mtu juu ya kufanya mambo mbalimbali"*.Ndani ya uwezo huu, kipo kipaji chako pia. Unazaliwa una kipaji tayari. Kumbuka tulisema kuwa kipaji ni uwezo wa kufanya mambo kwa ubora bila kutumia nguvu nyingi sana, na uwezo huu unakutofautisha na wengine.

Karama ipo tofauti sana. Hakuna anayezaliwa na karama. Mfano kwenye maandiko zinatajwa karama tisa zile atoazo Roho Mtakatifu **(1 Wakorintho 12:4 – 11)**, hakuna karama hata moja ambayo mtu huzaliwa akiwa nayo. Huzaliwi ukiwa na karama ya neno la maarifa au matendo ya miujiza ila ukiokoka tu na kuingia kwenye familia ya Mungu; Basi, unaweza pata mgawo wa karama za Roho Mtakatifu.

Uhusiano wako na Mungu ni muhimu kuliko kipaji; Kumbuka ni Mungu atoaye hicho kipaji ulichonacho, kukitumia nje ya uhusiano wako na Mungu ni hasara.

>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>

# SURA YA PILI

# NJIA 4 ZA KUGUNDUA KIPAJI CHAKO



> Anga ni kubwa sana kwa kila nyota kuonekana na wala nyota moja haijawai kuizuia nyingine kung'aa
>
> – Mch. Dickson Kabigumila

Siku moja nilisoma makala iliyoandikwa na Samuel Sasali, mkurugenzi wa kampuni ya Kiango Media. Makala hii ilikuwa na kile alichozungumza kwenye MentorShip Program ambazo huandaliwa na kufanyika kila mwisho wa mwezi na Joel nanauka, mwanzilishi wa kampuni ya Leadership Development Company na taasisi ya African Success Academy. Kwenye makala hii, Samuel Sasali alizungumza kuhusu unawezaje kugundua kipaji chako? Nilijifunza mambo 5 ya kumsaidia mtu kugundua kipaji alichonacho, kati ya hayo nitaeleza mambo 4;

## KUMWOMBA MUNGU

Kati ya jambo muhimu kujua, ambalo nimeeleza mwanzoni kabisa ni kuwa; *"kipaji ni zawadi mtu anayozaliwa nayo" na kwamba; "Mtoaji wa kipaji ni Mungu na hutoa kwa kila mtu". Kama hujui kipaji chako ni vema kumwendea Mungu na kumwuliza "Kipaji changu ni kipi?*" maana ndie anaejua, zaidi sana anaetoa kipaji yeye.

Mchungaji Rick Warren wa kanisa la Saddleback Church, mwandishi wa kitabu cha "The Purpose-driven life" ambacho kimeuza nakala nyingi sana duniani anataja njia mbili za kumsaidia mtu kuanza kugundua kusudi la yeye kuumbwa; ya kwanza ni kujiuliza-uliza maswali, na ya pili kumwuliza Mungu. Hata ukitaka kujua kipaji chako unaweza kutumia njia hizi mbili; ukaanza kujiuliza *"hivi mimi kipaji changu ni kipi?, uwezo wangu wa kipekee ni upi?"* ukiendelea kujiuliza, badae utaona umegundua kipaji chako. Joel Nanauka anasema kuwa kati ya maswali makubwa watu hujiuliza ni;"*Nimeumbwa kufanya nini*?". Mchungaji Rick anasema kuwa;*"Njia rahisi zaidi ya kujua kusudi la uvumbuzi fulani ni kumwuliza aliyevumbua*". Njia rahisi zaidi, tena iliyo nzuri ni kumwuliza Mungu kwani si wote waliojiuliza-uliza wakapata kujua vipaji vyao. Kumwuliza Mungu ni kumfuata aliyeumba hicho kipaji na kutaka kujua toka kwake zaidi. Badala ya kupoteza muda zaidi kujiuliza-uliza ni bora zaidi kwenda kwa Mungu moja kwa moja na kumwuliza.

## WATU WANAOKUZUNGUKA; NDUGU NA MARAFIKI

Samuel Sasali anasema;"*watu wa karibu wanao uwezo mkubwa wa kukuambia juu ya yale ambayo una uwezo (kipaji) nayo wa kipekee".* Ili wakuambie unaweza eneo fulani inabidi wakuone ukifanya.

Ukifanya umejifungia ndani hakuna mtu atakuona, hivyo uwezo wako utabaki umefichika. Kuna watu wamekufa na vipaji vyao kwa sababu tu hawakutaka kuvionyesha mbele ya wengine. Hofu, woga, kukosa uthubutu ndio hufanya watu kuficha uwezo wao.

Nakumbuka nilipokuwa kidato cha sita, baada ya kurudi nyumbani wakati wa likizo nilitamani kupata kazi yoyote ya kunipatia hela ila watu hawakuamini naweza kufanya kazi. Nilipoona hawaamini nina uwezo wa kufanya kazi, labda kwa sababu ni mwanafunzi, niliamua kujipa kazi mwenyewe ili waone nina uwezo. Nilianza kufyatua tofali za tope, kuchimba choo na kujenga bafu mwenyewe pale nyumbani kwetu. Watu walipoona naweza, nilipata dili za kutosha na nikaingiza hela ya kutosha. Nakumbuka dili langu la kwanza lilikuwa ni kumwaga zege, badae kuchimba msingi wa nyumba ikafuata kufyatua tofali za simenti. Umeona kitu hapa? Nilianza kufanya nikaonekana. Watu wanaokuzunguka wana macho ya kuona uwezo wako, fanya uonekane.

Nilipokuwa nasoma kitabu cha TIMIZA MALENGO YAKO cha Joel Nanauka nilikutana na habari moja ambayo nataka niseme hapa. Joel Nanauka anasema kuwa;*"nilipokuwa mdogo, mama yangu alipata tenda ya kuwafundisha Kiswahili wazungu wamisionari nyumbani kwao, na alikuwa akinichukua nifuatane naye. Kila wakati tulipofika kulikuwa na watoto wawili wadogo ambao walikuwa wanamwagiwa vifaa mbalimbalii vya plastiki na kuanza kuumba maumbo mbalimbali…….siku moja mama yangu alipouliza kusudi la ule mchezo wale wamisionari wakasema "kwa kuangalia uwezo wa kila mtoto anaweza kuunganisha vitu gani, huwa tunaweza kujua*

*tuanze kumuelekeza katika masomo gani yatakayoendana na kipaji chake……..*". Kwa hiyo kupitia kwa ndugu, marafiki na watu wengine wa karibu, watakwambia kipaji chako kila mara wakuonapo unafanya.

**MATATIZO.**

Mtu anaweza kugundua kipaji chake kupitia matatizo. Mara nyingi "*comfort zone*" huficha kipaji cha mtu. Kipaji kilichofichwa ndani ya mtu huibuliwa pale ambapo mtu huyo atapitia matatizo magumu ya kumfanya atoke kwenye comfort zone.

Matatizo kama kuachishwa kazi, kukataliwa huibua uwezo wa mtu uliofichwa. Kuna rafiki yangu fulani alifukuzwa chuo, baada ya muda niliona akijitangaza kuwa yeye ni mshehereshaji mzuri sana na kwa sasa anaingiza hela nyingi sana. Huenda asingefukuzwa chuo kipaji chake ingechukua muda kuonekana, kingemezwa na ajira baada ya kumaliza chuo, ila kule kufukuzwa chuo kulifichua kipaji chake. Inawezekana wewe ni mwandishi wa vitabu ila uwezo wako umefichwa na ajira inayokula muda wako. Inawezekana wewe ni mtoro kwenye kipaji chako cha utunzi wa nyimbo nzuri kwa sababu kaisari anakula muda wako wa kutulia na kukijua kipaji chako.

Wako watu wengi waliogundua vipaji vyao katikati ya matatizo. Iko habari moja kwenye biblia kumhusu jitu kubwa aliyeitwa Goliath. Kama si huyu Goliath, kijana aitwae Daudi asingejua uwezo wake wa kupigana. Goliath alikuwa ni tatizo kwa jeshi la Israeli, lakini kwa Daudi ilikuwa ni fursa ya kugundua uwezo wake kwani aliweza kulipiga hili jitu. Matatizo yanaweza kumpa mtu macho ya kuona

uwezo wake, na napenda hapa ninukuu alichowahi kusema Raisi wa tatu wa Israeli, Sulemani, kuwa "*...siku ya mabaya ufikiri...*". Kufikiri huku ndio hufungua muono ndani ya mtu wa kugundua kipaji chake.

## USHINDANI

Miaka ya nyuma shule zetu za msingi na sekondari kulikuwa na mashindano ya michezo ya kuibua vipaji vya wanafunzi. Bado mashindano haya kwenye shule za sekondari yanaendelea yakijulikana kama UMISETA. Kupitia ushindani mtu anaweza kugundua kipaji chake. Leo hii kuna mashindano kama Bongo Star Search, Gospel Star Search na MiaMia ambayo huibua vipaji mbalimbali vya vijana vilivyofichika. Inapotokea nafasi ya kushiriki mashindano ya kuibua vipaji usisite kushiriki, ni fursa kwako kuonesha uwezo wako na itafangua mlango wa kufanya kazi na wengine kwenye eneo la kipaji chako.

Ushindani kwenye soko la kipaji kile ulichonacho huweza kukupa kujua uwezo wako zaidi. Kila unapojua uwezo zaidi hukuchochea kufanya vizuri zaidi kuliko wengine. Kufanya vizuri zaidi ndio tafsiri ya ubora. Huwezi kufanya kikawaida na bado ukawepo kwenye kundi la wanaofanya kwa ubora. Ushindani huibua vipaji, usisahau hilo, usiogope kuingia kwenye ushindani.

>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>